

Taasisi ya Thirdmill Beji ya Tabia

“Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, Amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi”

Wagalatia 5:22, ESV

Mojawapo ya sifa Muhimu za kiongozi wa Kanisa au Huduma ni tabia ya kimungu. Maana ya Tabia katika Kamusi ni “Ni sifa za Kiakili na za Kimaadili zinazomtofausha mtu binafsi” basi hizi sifa za kiakili na Kimaadili ni tabia za Kimungu tunazoagizwa kuwa nazo Kupitia Neno la Mungu. Mfano Wagalatia 5. Hata hivyo, Mara nyingi katika huduma, watu wengi wanaokuja Kanisani, wanapenda sana mafundisho kuliko tabia ya Kimungu. Badala ya kukua utu wetu wa ndani, pamoja na tunda la roho, badala yake, matokeo ya huduma ndiyo yamepewa kipaumbele na sio kutazamia jinsi ya kukua katika tabia ya kimungu. Katika beji hii tutaulizia baadhi ya maswali kuhusu huduma zetu, maisha, na kuangalia jinsi ya kukua katika tabia ya kimungu.

Vipengele vya Beji:

Utamaduni na Tabia – ni nini ni mtazamo wa utamaduni na Biblia kuhusu mafanikio?

Wewe na Tabia yako – Je, unajifunza nini kuhusu uwezo na Udhaifu wetu wenyewe?

Ahadi za Mungu na Tabia yake – ni kwa jinsi gani ahadi na Neema za Mungu hujenga tabia ya kimungu?

1. Nini tafsiri ya mafanikio katika Utamaduni wako?
2. Nini tafsiri ya mafanikio katika Kanisa au Huduma?
3. Ni kwa njia zipi utamaduni wako unavyotafsiri mafanikio na kwa jinsi gani Kanisani kwako au huduma inavyotafsiri mafanikio ni sahihi au mbaya?
4. Ni nani anayetoa ufafanuzi sahihi wa mafanikio katika Huduma yako?
5. Tito 1:7 inatufundisha kwamba Kiongozi “asilaumiwe, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi au Mpenda mapato ya Aibu.”
6. Je, umewaona viongozi kanisani au kwenye huduma ambao hawakuzingatia sifa hizo hapo juu? Je, ni madhara gani yanalikumba Kanisani au huduma?
7. Tito 1:8, inasema kuwa kiongozi anatakiwa kuwa “mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu na mwenye kudhibiti nafsi yake.”
8. Je, makanisani unawaona viongozi wenye sifa hizi? Je, hili linaathiri kanisa au huduma kwa namna gani?
9. Unapokumbuka tunda la Roho na ukitazama sifa za kiongozi katika Tito 1, ni tabia gani unahitaji katika kukua?

10. Je, ukotayari ukikosolewa hasa kwenye jambo gumu, hasa kwenye maeneo ambayo wengine wanaona kuwa unahitaji kukua?
11. Je, unaukaribu na watu, kwamba watu wanaweza kuzungumza na wewe kwa ukaribu bila woga na kwa uaminifu? Watu walio karibu nawe wanasema kwamba unafikika?
12. Je, unakubali kukosolewa na watu?
13. Elezea ni wakati gani ulikubali kushughulikia ukosoaji vizuri na wakati ambao haukuweza kufanya vizuri.
14. Je, una mtu katika maisha yako ambaye anaweza kuwa mwaminifu kukuelezea maeneo ambayo unahitaji kukua
15. Ni maeneo gani katika maisha yako binafsi unafanya vizuri kitabia?
16. Je, una udhaifu katika maeneo gani kitabia?
17. Je, unaweza kuendelea kuwa mnyenyekevu kwenye maeneo ambayo unafanya vizuri kitabia?
18. Je, unasema nini juu ya maeneo uliyodhaifu kitabia na unayashughulikia kwa namna gani?
19. Je, unakumbana na changamoto gani kwenye maeneo unayoona umekua kitabia?
20. Je, ni changamoto gani unakumbana nazo kwenye maeneo ambayo ulikosea kitabia?

Hamna kitu cha msingi kwa viongozi zaidi ya kukumbushwa kila wakati juu ya uwepo, nguvu, ahadi na neema ya Mungu. Zawadi kubwa ya Mungu kwako sio mafunzo ya Seminari, theolojia au wito wa huduma yako. Bali zawadi kubwa kwenye maisha yako ni Mwanae Yesu Kristo.

1. Je, kukumbushwa mambo haya kumekusaidia kukua katika tabia na mahusiano yako na Mungu kwa kiasi gani?
2. Je, ni njia gani unazotumia katika maisha yako kujikumbusha kuhusu uwepo, nguvu, ahadi na neema ya Mungu?
3. Je, unaweza kujumuisha haya kwenye maisha yako ili kukusaidia kukua katika tunda la roho?

Mambo ya kufanyia kazi:

1. Kama huna mtu, tafuta mtu unayeweza kuzungumza naye mara kwa mara kuhusu jinsi unavyoendelea kukua katika tabia. Hakikisha ni mtu anayeweza kukuelezea bila woga ili ukue?
2. Toa mrejesho kwenye kundi lako mtu huyo nani, na uwaambie nini kimetokea kwenye mazungumzo kuhusu maisha yako?
3. Fikiria jinsi unavyoweza kukua kibinafsi hasa katika suala la tabia ya Kimungu. Tengeneza mpango na uandike, jumuishia mambo yanayoweza kukufanya kukua. Shirikisha jumuiya yako na omba maoni yao.